KUCHUNGUZA MBINU ZA KITANZIA ZA KI-ARISTOTLE KATIKA TAMTHILIYA ZA FUMO LIONGO NA SUNDIATA

SALOME MHANGILWA CLEMENCE

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2015

UTHIBITISHO

Aliyetia saini yake hapa chini, anathibitisha kuwa, amesoma tasnifu hii iitwayo ***"Itikadi katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo",*** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Digrii ya Uzamili (MA Kiswahili - Fasihi) katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……

Profesa, Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

……..……

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi ***Salome, Clemence Mhangilwa*** natamka ya kwamba hii ni tasnifu yangu mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya mahitaji ya kutunukiwa shahada kama hii au shahada nyengine.

……

Saini

…….

Tarehe

TABARUKU

Kazi ninaitabaruku kwa wazazi wangu kwa malezi bora walionilea mtoto wao nakunipeleka shule na kupata elimu pia naitabaruku kwa wanangu na iwe kumbukumbu yao.

SHUKURANI

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima, afya njema na ustahamilivu katika kipindi chote cha utafiti. Yeyote aliyewahi kufanya utafiti atakubaliana nami kwamba kufanya utafiti si kazi rahisi hata kidogo. Kwani misaada ya watu mbalimbali ya hali namali inahitajikavinginevyo unaweza ukatamauka na kazi ikakushinda. Nitakuwa si binadamu ninayejali utu, endapo nitashindwa kuwashukuru watu ambao wamechangia ukamilishajiwa kazi hii. Hata hivyo haitokuwa rahisi kuwatajawotekwa majina kwa sababu niwengi. Bali nitawataja wachache tu ili wawe ni wawakilishi wa wenzao.

Kwanza namshukuru mwalimu wangu na msimamizi wangu wa utafiti huu Profesa. Emmanuel Mbogo ambae kwa asilimia kubwa ndie alienisaidia tokea nilipowasilisha wazo la utafiti, kuandika pendekezo, kufanya utafiti hadi uandishi wa tasnifu hii. Kwa busara na hekima aliniongoza, alinishauri na kunikosoa kila palipostahili bila kuchoka wala kukimwa. Kwahakika alijitahidi kutimiza wajibu wake katika kusimamia kazi hii pamoja na majukumu mengi ya kitaaluma, kifamilia, na ya kijamii yanayomkabili. Ama kwa hakika kutoka kwake nilipata mengi ya kiutafiti, usimamizi na usaidizi wake haupimiki wala haulipiki abadani. Lengo ni kumuomba Mwenyezi Mungu ambariki kwa kumjaalia uzima, afya njema na mafanikio mema katika kazi zake.

Pia napenda kumshukuru Mwalimu wangu muongozaji na msaidizi wangu wa kazi hii mwalimu Prof. T. S. Y. M Sengo kwa kunijali kunipa msaada wake wa hali na mali , si usiku si mchana ,si mvua sijua, alinipa msaada wake Mwenyezi Mungu

amjalie maisha marefu yenye Amani na Baraka tele juu yake. Aidha shukurani nyengine ziwaendee ndungu zangu wa familia kwa ushauri wao wa hali na mali pia natoa shukurani zangu kwa wale walioshiriki kunipatia data za utafiti. Itakuwa ni muhali kwangu kusahau kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia, mume wangu ,watoto wangu kwa upendo na uvumilivu mkubwa waliouonyesha wakati nikiwa masomoni na katika kipindi utafiti. Uvumilivu wao ulinipa matumaini na utulivu wa kuendelea na masomo vizuri. Ahsanteni nyote.

IKISIRI

Kazi hii ilihusika na mada inayohusiana na Kuchunguza mbinu za kitanzia za Ki-Aristotle katika Tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata*. Malengo mahususi ya utafiti huu yalikuwa ni kuchambua matumizi ya mbinu za tanzia za Kiaristotle katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* na Sundiata, kuelezea matumizi ya mbinu ambazo si za tanzia za *Ki-Aristotle katika tamthiliya teule* na kuchambua dhamira katika tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata*. Data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya tanzia ya Ki-Aristotle. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, mbinu za Ki-Aristotle zinazojitokeza katika tamthiliya teule ni msuko, wahusika, dhamira, fikra, utumiaji wa jukwaa na mtungo wa tamthiliya. Mbinu zisizo za Ki-Aristotle ni utendi, usimuliaji, diolojia, monolojia, majigambo na kuchanganya ushairi na nathari. Kwa upande wa dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya teule ni uongozi kandamizi, rushwa katika jamii, usaliti, matabaka, nafasi ya mwanamke na ushirikina katika jamii.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **viii**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI KWA UJUMLA **1**

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti 1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti 2

1.4 Malengo ya Utafiti 3

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti 3

1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti 3

1.4.3 Maswali ya Utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 4

1.6 Mipaka ya Utafiti 5

1.7 Hitimisho 5

SURA YA PILI **6**

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA **6**

2.1 Utangulizi 6

2.2 Tamthiliya kwa Ujumla 6

2.2.1 Historia ya Tamthiliya 6
2.2.2 Wakati wa Ukoloni 7
2.2.3 Baada ya Uhuru 7
2.2.4 Uhakiki wa Tamthiliya 7
2.3 Wahakiki wa Kazi za Emmanuel Mbogo 8
2.4 Pengo la Maarifa 8
2.5 Mwega wa Nadharia ya Utafiti 9
2.5.1 Mikondo ya Tanzia 9
2.5.1.1 Tanzia ya Urasmi 9
2.5.1.2 Tanzia ya Urasmi Mpya 10
2.5.1.3 Tanzia ya Kisasa 10
2.5.1.4 Tanzia ya Uhalisia wa Ujamaa 11
2.5.1.5 Nadharia ya Ki-Aristotle/Urasmi Mkongwe 12
2.6 Hitimisho 14
SURA YA TATU 15
MBINU ZA UTAFITI 15
3.1 Utangulizi 15
3.2 Usanifu wa Utafiti 15
3.3 Eneo la Utafiti 16
3.4 Kundi lengwa na Sampuli ya Utafiti 16
3.4.1 Sampuli na Usamplishaji 17
3.4.2 Usamplishaji 17
3.4.3 Sampuli 17
3.5 Vyanzo vya Data 18

3.5.1 Data za Msingi 18
3.5.2 Data za Upili 18
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data 19
3.6.1 Usomaji Makini 19
3.7 Uchambuzi wa Data 20
3.7.1 Mkabala wa Kidhamira 20
3.8 Usahihi wa Mbinu za Utafiti 21
3.8.1 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti 21
3.8.2 Maadili ya Utafiti 22
3.9 Hitimisho 22
SURA YA NNE 23
UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI 23
4.1 Utangulizi 23
4.2 Mbinu za Tanzia za Ki-Aristotle, Zisizo za Ki-Aristotle na Dhamira katika Tamthiliya ya Fumo Liongo 23
4.2.1 Mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika Tamthiliya ya Fumo Liongo 24
4.2.1.1 Msuko 24
4.2.2 Wahusika 25
4.2.3 Dhamira 25
4.2.4 Fikra 26
4.2.5 Mtungo wa Tamthiliya 27
4.3 Mbinu zisizo za Ki-Aristotle Katika Tamthiliya ya Fumo Liongo 27
4.3.1 Mbinu za Utendi 28
4.3.1.1 Mbinu ya Usimuliaji 28

4.3.1.2 Mbinu ya Diolojia 28
4.3.1.3 Mbinu ya Monolojia 29
4.3.2 Mbinu ya Majigambo 29
4.3.3 Mbinu ya Kuchanganya Ushairi na Nathari 29
4.3.3.1 Utangulizi 29
4.4 Maudhui katika Tamthiliya ya Fumo Liongo 30
4.4.1 Uongozi Kandamizi 30
4.4.2 Rushwa 31
4.4.3 Usaliti 31
4.4.4 Matabaka 31
4.4.5 Nafasi ya Mwanamke katika Harakati za Ukombozi 32
4.5 Hitimisho 32
4.6 Mbinu za Tanzia za Ki-Aristotle, zisizo za Ki-Aristotle na Dhamira katika Tamthiliya ya Sundiata 32
4.6.1 Mbinu za Ki-Aristotle katika Tamthiliya ya Sundiata 33
4.6.1.1 Msuko 33
4.6.1.2 Wahusika 33
4.6.1.3 Dhamira 34
4.6.1.4 Fikra 35
4.6.1.5 Mtungo wa Tamthiliya 35
4.6.2 Mbinu Sisizo za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya Sundiata 36
4.6.2.1 Mbinu ya Utendi 36
4.6.2.2 Mbinu ya Usimuliaji 36
4.6.2.3 Mbinu ya Dialojia 37

4.6.2.4 Mbinu ya Monolojia 37

4.6.2.5 Mbinu ya Majigambo 37

4.6.2.6 Mbinu ya Kuchanganya Ushairi na Nathari 38

4.6.2.7 Mbinu ya Uchawi na Uganga 38

4.6.2.8 Mbinu ya Nyimbo na Ngoma 39

4.6.3 Dhamira katika Tamthiliya ya Sundiata 39

4.6.3.1 Uongozi Mbaya 40

4.6.3.2 Rushwa 40

4.6.3.3Nafasi ya Mwanamke katika Jamii 40

4.6.3.4 Ushirikina 41

4.7 Hitimisho 42

SURA YA TANO 43

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 43

5.1 Utangulizi 43

5.2 Muhtasari 43

5.2.2 Mbinu za Ki-Aristotle katika Tamthiliya Teule 43

5.2.3 Mbinu Sizizo za Ki-Aristotle 44

5.2.3 Dhamira katika Tamthiliya Teule 44

5.3 Hitimisho 45

5.4 Mapendekezo 45

MAREJELEO 46

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI KWA UJUMLA

1.1 Utangulizi

Hii ni sura tangulizi inayobainisha tatizo la utafiti lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu. Kwa hiyo, sura hii inabainisha na kuelezea usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti Malengo ya utafiti, mipaka ya utafiti, Maswali ya utafiti ambayo utafiti huu ulikusudia kuyajibu na Umuhimu wa utafiti.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kazi hii inachunguza mbinu za tanzia za Ki-Aristotle, kwa kutumia tamthiliya ya Fumo Liongo na Sundiata zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo. Tunachunguza jinsi mwandishi alivyotumia vilivyo mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika kazi zake za fasihi, kazi hizi mbili zimechaguliwa kwa kuwa zina Misingi katika Fasihi Simulizi hasa Utendi – Simulizi. Fumo Liongo ni tamthiliya iliyotokana na Utendi-Simulizi wa Afrika Mashariki uitwao Fumo Liongo (katika Pwani ya Kenya na Tanzania). Sundiata pia ni tamthiliya inayotokana na Utendi – Simulizi wa Afrika Magharibi uitwao Sundiata. Hadithi hizi zinasawiri Ubatili wa kuwania Mamlaka (Mulokozi 2011).

Aristotle (1958) katika kitabu cha *Poetics* anaelezea dhana ya tanzia, kuwa ni tamthiliya yenye huzuni inayogusia hisia za watazamaji kiasi cha kuogopesha na kumuonea huruma mhusika mkuu ambaye atapata janga. Tamthiliya hizi zinatupa mwanga kuhusu dhana hii ya tanzia.

Tilak (1990), anasema huzuni na hofu katika tanzia husababishwa na matukio kama yatafanywa na wanafamilia. Pia huweza kusababishwa na tendo linalofanywa kwa kujiamini sana mfano, *Fumo Liongo*, au tendo la kujiamini sana mfano, *Sundiata*, Kwa hiyo uoga na kihoro husababishwa na tukio la kutisha mfano kifo cha *Fumo Liongo au Sundiata*. Matukio haya husababishwa na kujiamini sana hivyo ukosefu wa maarifa ya kuelewa hatari iliyopo mbele yake (Harmatia). Janga analopata mhusika mkuu, huamusha hisia ya uoga unaotokana na harmatia au ukosefu wa maarifa.

Njogu na Chimerah (1999), wanasema, Aristotle (1958), alitambua vipengele sita vya kazi za tamthiliya ya Kigiriki ambavyo ni; (i) Nyimbo (ii) Matamshi (iii) Mtiririko wa vitendo (iv) Wahusika (v) Fikra na (vi) Utumiaji wa Jukwaa. Pia aliigawa tamthiliya ya Kigiriki katika sehemu tatu: (a) Utangulizi (Kianzio) (b) Kitendo (c) Wimo wa tamati (Hitimisho au kimalizio), Huu ndio muundo wa tamthiliya za Kigiriki. Muundo huu umewaathiri watunzi wengi sana wa tamthiliya za Kiswahili akiwemo mwandishi Emmanuel Mbogo. Mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, kijamii na kimazingira pia yamemuasili mwandishi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo na Sundiata* na kusababisha mwandishi akiuke mbinu zingine za tanzia za Ki-Aristotle. Utafiti huu umeainisha mbinu za tanzia za Ki-Aristotle na zile ambazo si za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya *Fumo Liongo na Sundiat.*

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Edwin Semzaba (1997), akimnukuu Aristotle (1958), anasema tanzia ni tamthiliya yenye huzuni inayogusa hisia za watazamaji kiasi cha kuogopesha na kumuonea

huruma mhusika mkuu anayepata janga. Watafiti wengi wa kazi za tamthiliya wamevutiwa sana katika kutafiti vipengele vya kifani na kidhamira katika kazi hizo. Miongoni mwa watafiti hao ni Ligembe (1995), Mwaifuge (2001), Mlama (2003), Hussein (2003), Ramadhan (2005), Mwita (2009) na Nicholous (2011). Watafiti hawa wamevutiwa sana na utunzi wa tamthiliya za majaribio na kumakinika katika kuhakiki na kutafiti vipengele hivyo katika tamthiliya ya Kiswahili. Hakuna mtafiti hata mmoja kati ya hawa ambaye amechunguza matumizi ya mbinu za Kiaristotle katika tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata*. Hili ndilo tatizo la utafiti ambalo utafiti huu umekusudia kulichunguza.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una jumla ya lengo kuu moja na malengo mahususi matatu ya utafiti. Malengo haya ni kama yafuatayo:

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya za *Fumo Liongo na Sundiata.*

1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

Utafiti huu una jumla ya malengo mahsusi matatu, na malengo hayo ni:

(i) Kubainisha matumizi ya mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* na *Sundiata*.

(ii) Kubainisha matumizi ya mbinu ambazo si za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya teule.

(iii) Kubainisha dhamira zinazoibuliwa kutokana na matumizi ya mbinu za Ki-Aristotle katika tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata*.

1.4.3 Maswali ya Utafiti

(i) Mbinu zipi za tanzia za Ki-Aristotle zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* na *Sundiata*?

(ii) Ni mbinu zipi zisizo za Ki-Aristotle zinazojitokeza katika tamthiliya teule?

(iii) Ni dhamira gani zinazojibainisha katika tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata*?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu kitaaluma utachochea mijadala mbalimbali ya kitaaluma inayohusu tamthiliya ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu wa kuchunguza mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya Kiswaihili kwa hakika utaleta mjadala adhibu katika taaluma ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa ujumla.

Utafiti huu utaongeza idadi ya Marejesho kwa Watafiti mbalimbali; Vyuo Vikuu, Maprofesa, Wahadhiri wa taaluma ya Fasihi ya Kiswahili katika uandishi wa vitabu na makala mbalimbali. Wanafunzi kwa upande wao watauona, utafiti huu kuwa wa manufaa kwao katika kutafuta tatizo la utafiti ili kuimarisha sehemu ya mapitio ya kazi tangulizi katika tafiti zao. Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa sana kwa vyombo mbalimbali na ukuzaji, uendelezaji wa kazi za sanaa kama vile: Tamthiliya, Filamu, Muziki na Ngoma na Vyombo kama Baraza la Sanaa la Tanzania pamoja na Bodi ya Filamu ya Sanaa Tanzania. Baada ya kuchunguza mbinu za tanzia za Ki-

Aristotle katika tamthiliya teule, vyombo hivi vitapata utajiri mkubwa sana wa mafunzo na elimu mbalimbali iliyomo katika tamthiliya teule. Hivyo itakuwa rahisi kwao kuandaa mikakati na sera madhubuti ya kukuza utunzi wa tamthiliya nchini Tanzania.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kuchunguza mbinu za tanzia za Ki-Aristotle peke yake katika tamthiliya teule. Utafiti huu pia unalenga vitabu viwili tu vya Emmanuel Mbogo ambavyo ni *Fumo Liongo* na *Sundiata* ingawaje mtunzi huyu ana vitabu vingi. Utafiti huu utajikita katika tamthiliya hizi tu kwa kuwa zote zina misingi ya tenzi – simulizi za Kiafrika.

1.7 Hitimisho

Katika Sura hii, msingi wa utafiti umewekwa ambao ni kuchunguza mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* na *Sundiata* za Emmanuel Mbogo zilizoteuliwa. Imejadili: Usuli wa tatizo la Utafiti, Tamko la tatizo la Utafiti, Malengo ya Utafiti, Lengo la Jumla, Malengo Mahsusi na maswali ya Utafiti. Katika Sura inayofuata tutajadili Mapitio ya kazi tangulizi na Mkabala wa Kinadharia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumefanya mapitio ya kazi tangulizi ambazo zinahusiana na mada ya utafiti huu. Mapitio ya kazi tangulizi yamefanywa kwa lengo la kumwezesha mtafiti kubaini pengo la maarifa ambalo yeye amelishughulikia katika utafiti wake. Katika kufanya kazi ya kupitia machapisho mbalimbali tumeanza na yale yaliyozungumzia tamthiliya kwa ujumla.

2.2 Tamthiliya kwa Ujumla

Katika sehemu hii tumepitia kazi zilizoelezea historia ya tamthiliya tangu ilipoanza mpaka hivi leo.

2.2.1 Historia ya Tamthiliya

Watafiti kadhaa wamefanya utafiti na kuandika tasnifu zao kuhusu tamthiia za Kiswahili kwa madhumuni mbalimbali miongoni mwa maudhui hayo ni historia ya tamthiliya ya Kiswhaili Kabla ya Ukoloni, Wakati wa Uhuru na Baada ya Uhuru. Kabla ya kuja kwa wakoloni, Tamthiliya hazikuwepo, badala yake zilikuwepo sanaa za maonesho ambazo ni Ngoma na Hadithi ambazo ndizo msingi wa maigizo na zilikuwa simulizi (Mlama (1976; Mbogo, 1997; Mulokozi, 1996 na Eliakimu, 1987). Tamthiliya ilianza Tanzania wakati wa ukoloni kupitia taasisi kama shule, tamthiliya hizi zilijaa itikadi za kibepari mfano ni tamthiliya za Kiingereza; *The Sherrif's Kitchen na The Ugly Ducling ya Milne*, kwa ajili ya kuburudisha watawala na kumdhalilisha mtawaliwa (Bertoncini, 1989).

Kwa mujibu wa Wafula (1999), anasema tamthiliya za baada ya Uhuru ni tamthiliya za kisasa zilizozuka kutokana na maigizo ya kijadi zenye lengo la kujikomboa na ukoloni mkongwe na sasa ukoloni mamboleo mfano wa tamthiliya hizi ni *The Trial of Brother Jero ya Wole Soyinka na ile ya Medicine for Love ya Henshow* tutaitumia historia hii ya tamthiliya ya Kiswahili katika utafiti wetu kwa lengo la kukamilisha utafiti wetu.

2.2.2 Wakati wa Ukoloni

Bertoncini (1989), Penina Muhando Mlama (1983), na Eliakimu (1987), wanakubaliana kwa pamoja kwamba Waingereza wakati wa utawala wao walileta tamthiliya yao kwa lugha ya Kiingereza mfano: michezo ya Shakespeare ambayo ilitafsiriwa kwa Kiswahili na ilitungwa kwa lengo la kumdunisha Mwafrika.

2.2.3 Baada ya Uhuru

Wafula (1999) anasema tamthiliya za baada ya uhuru ni tamthiliya za kisasa zilizuka kutokana na maigizo ya kijadi yaliyokuwa na lengo la kujikomboa na ukoloni mkongwe na sasa ukoloni mamboleo. Kwa hiyo kutokana na historia ya tamthiliya, tutaitumia historia hii ya Kiswahili katika utafiti wetu kwa lengo la kukamilisha utafiti wetu.

2.2.4 Uhakiki wa Tamthiliya

Tamthiliya ya Kiswahili imehakikiwa na wahakiki wengi kama vile:- Senkoro (2001) alifanya utafiti kuhusu fasihi ya majaribio, aligundua kuwa fasihi ya majaribio ni fasihi inayochangaya tanzu za Fasihi simulizi na Fasihi Andishi mfano, katika

tamthiliya ya S.A. Mohamed *(Kivuli Kinaishi)* ili kujenga maudhui ya kazi yake, Mawazo ya Senkoro tunayafanyia kazi katika utafiti wetu, ili kuukamilisha.

Mulokozi (1996) alifanya utafiti katika Drama – Tendi (Epic Theatre) ya Bertolt (1980) aligundua mbinu ya kutumia historia ya zamani na matukio ya mbali ili kuwazindua watu wa leo. Utafiti wake umetusaidia katika uchambuzi wa data ili kukamilisha utafiti wetu. Semzaba (1997) alifanya utafiti katika tamthiliya za *Kinjeketile, Hatia na Mkwawa Mahinya* aligundua kuwa zilikuwa na umbo la asilia la Ki-Aristotle. Uchunguzi huu uliofanywa na wataalamu hawa utatusaidia katika uchambuzi wa data za utafiti wetu.

2.3 Wahakiki wa Kazi za Emmanuel Mbogo

Wahakiki kadhaa wamehakiki tamthiliya za Emmanuel Mbogo, kwa mfano, Kimani Njogu na Rocha Chimerah (1999), wamechambua tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi,* wamegundua matumizi ya uchawi na urogi kama mihimili mikuuu ya tamthiliya hii, imetumika kama jambo la uongozi wa kisiasa wa Kiafrika na uhusiano uliopo baina ya viongozi na wanaoongozwa.

Edwin Semzaba (1997) alifanya utafiti katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo ya *Morani na Ngoma ya Ng'wanamalundi* aligundua matumizi ya uchawi na uganga ili ziwe karibu na utamaduni wa Mwafrika. Uhakiki wa wataalamu hawa katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo utatusaidia katika utafiti wetu.

2.4 Pengo la Maarifa

Baada ya kuchunguza kwa kina tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu uchunguzi wa mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika kazi mbalimbali za fasihi, Utafiti huu,

umebaini kuwa zimejikita katika uchunguzi w masuala mengine mpaka sasa hakuna utafiti wa kina kuhusu uchunguzi wa mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* na *Sundiata*. Pengo hili ndilo ambalo utafiti huu umekusudia kuliziba.

2.5 Mwega wa Nadharia ya Utafiti

Wataalamu mbalimbali wamefasili nadharia kuwa ni kauli za kisanyansi zitokanazo na matokeo ya muda mrefu ya utafiti juu ya tatizo moja hilo hilo. Wamitila (2008) ameeleza nadharia yaweza kuwa kiini, wazo au mawazo ya mtu mmoja au kundi la watu. Owhida (2006) anasema nadharia ni mawazo ya mtu mmoja au kundi la watu kuhusu jambo au kitu ambacho kinaweza kuwa mwelekeo wa watu, jamii, kundi la watu au mtu mmoja mmoja na kusaidia kupata ukweli au kuthibitisha ukweli wa jambo kwa lengo maalumu lililokusudiwa.

2.5.1 Mikondo ya Tanzia

Wamitila (2003) anasema nadharia ya tanzia ni mawazo ya kimsingi ya Mnyunani aliyejulikana kama Aristotle, Mawazo haya yalijengwa kwenye muundo wa tanzia. Historia ya Umbo la tanzia imo katika mikondo ya tanzia kama ifuatavyo:

(1) Tanzia ya Urasmi

(2) Tanzia ya Urasmi Mpya

(3) Tanzia ya Kisasa

(4) Tanzia ya Uhalisia ya Ujamaa

2.5.1.1 Tanzia ya Urasmi

Hii ni tanzia ambayo ilitokana na tabaka tawala huko Ugiriki. Katika tanzia hii, mhusika mkuu sharti awe na tabaka tawala, anapata janga ambalo humtoa katika hali

ya juu na kuwa duni. Tanzia hii huonyesha huruma, hofu na majonzi. Miungu ilikuwa na kauli ya wema/uovu katika dunia. Mhusika mkuu alikuwa hawezi kushindana nazo. Lugha iliyotumika ni ya kishairi. Kuna utenganisho wa Waigizaji na Watazamaji. Pia kulikuwepo na mwitikio (korasi) kama uwepo wa demokrasia. Mfano wa tamthiliya hiyo ni *Mfalme Edipode (1971).*

2.5.1.2 Tanzia ya Urasmi Mpya

Ni tanzia iliyotokana na tabaka tawala huko Uingereza lililomiliki sanaa. Mhusika mkuu alikuwa wa ukoo bora, nafasi ya Mungu wa Mashetani iliendelea kuwepo. Lugha iliyotumika ni ya kishairi kwa watu wa Juu, watu wa chini waliongea lugha ya kawaida.

Shakespeare (1564 – 1616), aliona tanzia kuwa ni sababu ya uovu ambao mtu humutendea mwingine, alizingatia zaidi dhamira yake mwenyewe, mfano mzuri ni tamthiliya ya *Hamlet (1958).*

2.5.1.3 Tanzia ya Kisasa

Hii ni tanzia iliyotokana na mabadiliko ya fikra na maisha. Huu ulikuwa wakati wa ubepari huko Ulaya Karne ya 18, ulikuwa wakati wa mapinduzi ya viwanda, watu wengi walikimbilia mjini kwa hiyo hali mbovu za maisha zilijitokeza. Wafanyakazi waliweza kufahamu unyonyaji uliokuwa ukiendelea. Mhusika mkuu aliyekumbwa na janga alitoka ngazi yoyote ya jamii. Lugha iliyotumika ni ya kawaida ili kurahisisha mawasiliano, ni lugha iliyoounganisha mwigizaji na mtazamaji *(Carthasis),* ilibaki kuwa kiini kikubwa cha tanzia ya kisasa kama katika mikondo mingine iliyopita.

Hata hivyo, *Henrik Ibsen (1828 – 1906),* anasema kuwa kuangamia kwa mhusika mkuu ni fundisho kwa jamii kuwa jamii inaweza kupata mwisho mzuri ikiwa itabadilisha hali mbaya ya maisha kuwa nzuri, au kutokana na mawazo ya kidini ya maisha baada ya kifo. Tanzia hii ya kisasa ilionesha jinsi misingi potovu ya jamii ilivyounganisha watu mfano mzuri ni katika tamthiliya ya *Ghost (Mashetani (1965) ya Henrich Ibsen* ambaye ilionyesha matukio yaliyosababishwa na jamii kushurutishwa kufuata maadili potovu. *Tanzia ya Kifo cha Mfanyabiashara (1949) ya Miller A.* ni mfano mwingine wa tanzia ya kisasa. Tanzia hii inaonesha kuwa mafanikio ni utajiri na Miller A anaamini kwamba mtu hawezi kupendwa bila kuwa na mafanikio.

Hata hivyo, Ibsen aliishambulia ndoa na maisha ya familia kuwa ndio chanzo cha hali ngumu kwa wahusika (A DOLL'S HOUSE 1879). Pamoja na mawazo ya Steiner, kuwa mhusika mkuu wa tanzia ya kisasa haangamii kwa sababu majibu ya matatizo yapo lakini uovu bado huendelea kuchipuka na kusababisha majanga. Tanzia za Kiafrika huchanganya Limino na Liminoid kwa kuwa na kuna nafasi ya Mungu na Mizimu katika maisha ya wakati huu mfano ni *Kinjeketile*. Hata hivyo tanzia za kisasa zinaonyesha muelekeo tofauti kutokana na mawazo ya binadamu kutokuwa na mipaka.

2.5.1.4 Tanzia ya Uhalisia wa Ujamaa

Tanzia hii imetokana na mawazo ya Marx na Ukoministi karne ya 16 kutaka kuleta jamii isiyo na matabaka duniani, Mhusika mkuu lazima autangaze ujamaa duniani bila kushindwa. Tanzia hii inaonyesha jinsi jamii nzima inavyobadilika kuwa ya

kikoministi. Mwisho wa tanzia ni mzuri kwa ushindi wa ujamaa. Mawazo yaliyotawala tanzia hizi yalitokana na chama cha kikoministi huko Urusi, fikra zilizolazimishwa kwa jamii kupokea mawazo wasiyoyapenda, kwa hiyo toka mwanzo ukandamizaji wa haki za binadamu upo katika tabaka za wakati wa Wagiriki, Shakespeare na hata sasa katika jamii zetu za Kiafirka.

Lugha iliyotumika ni ya kawaida ili kuleta maelewano bora kati ya waigizaji na watazamaji. Pia utengano maalumu kati ya waigizaji. Mhusika mkuu ni wa kipropaganda kwa manufaa ya siasa ya kikoministi ana sifa zifuatazo:-

(i) Ni mfano kati ya mifano

(ii) Amefikia kiwango cha juu zaidi cha ubinadamu

(iii) Hana makosa yoyote

(iv) Ni mwenye kuelewa siasa barabara

(v) Awe na akili

(vi) Awe na moyoshupavu

(vii) Awe na uzalendo

(viii) Aheshimu wanawake

(ix) Awe tayari kujitoa mhanga

(x) Awe na msimamo mmoja tu kufikia kilele cha Ukoministi asichanganye weupe na weusi. Huikwepashidha ili kulifikia lengo lake. (Semzaba (1997). Miungu hawana nafasi katika tanzia hizi.

2.5.1.5 Nadharia ya Ki-Aristotle/Urasmi Mkongwe

Nadharia ya Ki-Aristotle ni nadharia ambayo wasanii wengi wa michezo ya kuigiza huko Ulaya wameitumia kama mwongozo. Chimbuko la nadharia hii ni katika

kitabu kiitwacho *Poetics* cha *Aristotle*. Kiini cha nadharia hii ni sheria na kanuni za utunzi wa tamthiliya. Nadharia hii huugawa mchezo wa kuigiza wa tanzia katika vipengele sita (i) msuko (ii) wahusika (iii) dhamira (iv) utenzi wa matumizi ya maneno (v) nyimbo na (vi) maonesho.

Aristotle (1958), pia aliugawa mchezo katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni mwanzo au utangulizi. Sehemu ya pili ni kitendo chenyewe. *Aristotle* anapendelea uibwe katika sehemu ya tatu. *(Hussein 1983). Wamitila (2002),* anasema kuwa, nadharia ya tanzia ni mawazo ya kimsingi ya Myunani aliyejulikana kama *Aristotle*. Mawazo haya yalijengwa katika muundo wa tanzia. Mawazo ya *Aristotle* yamefanyiwa marekebisho fulani kutokana na sababu kuwa fasihi hubadilika.

Mawazo haya yanaungwa mkono na Hussein (1983), anayaeleza mabadiliko yaliyofanywa katika vipengele mbalimbali alivyovitambua Aristotle kwa mfano Shakespeare katika tamthiliya ya *(King-Lear),* kichaa *(fool)* ndiye anaimba mara kwa mara. *Ceiseire* katika tamthiliya ya A Season in the Kongo ametumia nyimbo katika sehemu mbalimbali.

Ngungi wa *Thion'go* katika tamthiliya ya *(Dedan Kimathi)* anatumia nyimbo hata mwanzoni mwa mchezo. Soyinka katika tamthiliya ya (The Swamp Dwellers), *P. Mhando* katika tamthiliya ya *(Pambo), Zola, Stindberg na Ibsen*, wametumia mazungumzo ya kitamthiliya *(Dramatic Dioloque),* kama kiwakilishi cha kuendesha tamthiliya na kusukuma mwanzo wa mchezo na mwisho, pia kitendo cha kati badala ya umbo la mizani kwani mazungumzo huonesha hali (mood).

2.6 Hitimisho

Sura hii inaelezea mikondo ya tamthiliya za kitanzia na sifa zake. Nadharia ya tanzia ya Ki-Aristotle/Urasmi Mkongwe iliyo na uhusiano wa karibu na mkondo wa tanzia ni muafaka katika kufanikisha utafiti wetu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumewasilisha na kueleza mbinu mbalimbali za utafiti ambazo zimetumika kukusanya na kuchambua data. Kothari (2008) anaeleza kwamba, mbinu za utafiti ni muhimu katika utafiti wa kitaaluma kwa sababu kutokana na mbinu hizi ndipo utafiti hufanyika kisayansi na siyo kiubabaishaji. Kwa kulifahamu hili, katika sura hii tumewasilisha mbinu mbalimbali za utafiti kama ifuatavyo:

3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu ni mbinu ya utafiti inayotumiwa na watafiti kuelezea picha, mchoro au ramani kamili juu ya namna utafiti huo utakavyofanyika (Babbie, 1999). Kimsingi zipo aina mbalimbali za usanifu wa utafiti lakini kwa minajili ya utafiti tumeteua uchunguzi kifani kuwa ndiyo aina ya usanifu wa utafiti iliyotumika katika kukusanya data za utafiti. Uchunguzi kifani ni aina ya usanifu utokanayo na mtafiti kuteua mahali au kitu maalumu ambacho anakishughulikia katika utafiti wake. Katika kazi hii tumeteua vitabu viwili vya tamthiliya ambavyo ni *Fumo Liongo* na *Sundiata* kuwa ndio uchunguzi kifani wetu ambapo tutapata data za msingi za utafiti wetu.

Robson (2007) anaeleza kuwa uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya kumwezesha mtafiti kutumia muda wake vizuri kwa kuwa tayari ameshateua kitu au vitu maalumu vya kushughulikia. Hii itamfanya asipoteze muda mwingi kwenda kushughulikia mambo ambayo hayahusiki katika utafiti wake. Pia, mbinu hii ni nzuri kwa sababu humwezesha mtafiti kutumia gharama ndogo itakayomwezesha kukamilisha utafiti

wake. Hivyo basi, kutokana na faida za usanifu wa kiuchunguzi kifani tumeiteua mbinu hii ili tuweze kukusanya data katika tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata*.

3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unakusudiwa kufanyika ili kuweza kupatikana kwa data za utafiti husika na kutimiza malengo yake (Young, 1984). Utafiti huu ulifanyika katika jiji la Dar es Salaa ambapo kunapatikana maktaba mbalimbali kama vile zile za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na Makavazi yake.

Maktaba hizo ndizo zimetumika katika kukusanya data za Upili za Utafiti wetu. Maktaba hizi kimsingi zimetusaidia kutupatia makala, vitabu, majarida na tasnifu mbalimbali ambazo zipo katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, sehemu ya East Afrikana pamoja na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

3.4 Kundi lengwa na Sampuli ya Utafiti

Populesheni ni idadi ya watu au vitu ambavyo mtafiti amevitumia kama watafiti wake. *Yin (1994)* anaeleza populesheni kuwa ni mkusanyiko wa watu au vitu katika hali na mazingira tofauti ambavyo hutoa data za utafiti husika. *Cooper (1989) na Varis (1990)* wanasema Populesheni ni wanachama wote, mtu mmoja mmoja, kikundi au element, ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Populesheni ya utafiti huu ni tamthiliya zote za Emmanuel Mbogo. Mtafiti aaliamua kuteua tamthiliya hizi kwa sababu aliamini kuwa ndizo ambazo zinaweza kumpatia data za utafiti alizozihitaji.

3.4.1 Sampuli na Usamplishaji

Kothali (2004) anasema, Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa, ulilochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo, ili atoe majumuisho ya utafiti wake. Usampulishaji ni mchakato unaohusisha mbinu mbalimbali za utenzi wa utafiti kwa lengo la kumpatia mtafiti taarifa ambazo alizitumia kwa kutoa majumuisho yanayowakilisha kundi kubwa la watafitiwa. Utafiti huu umetumia aina ya Sampuli Lengwa ambayo wakati mwingine hujulikana kama Sampuli Madhumuni. Sampuli Madhumuni ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huteua watafitiwa wake akiwa anatambua kwamba watamsaidia kupata data anazozihitaji ili kujibu maswali yake ya utaifi (Cresswell, 2000). Sampuli Lengwa ndiyo iliyotumika katika kupata data katika tamthiliya mbili teule kwa sababu tunafahamu fika kwamba kutokana na sampuli hii tutafanikiwa kupata data muafaka za kujibu maswali ya utafiti.

3.4.2 Usamplishaji

Kwa mujibu wa Kothari (2004) anasema, usamplishaji ni mchakato unaohusisha mbinu mbalimbali za uteuzi wa autafiti kwa lengo la kumpatia mtafiti taarifa ambazo zilitumika kwa kutoa majumuisho yanayowakilisha kundi kubwa la watafitiwa.

3.4.3 Sampuli

Kothari (2004) anasema, sampuli ni kundi dogo la watafitiwa waliochaguliwa kuwakilisha sifa mbalimbali na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili atoe majumuisho ya utafiti wake. Utafiti huu umetumia aina ya sampuli lengwa ambayo wakati mwingine hujulikana kama

sampuli madhumuni. Sampuli madhumuni ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huteuwa watafitiwa wake akiwa anatambua kwamba watamsaidia kupata data anazohitaji ili kujibu maswali yake ya utafiti (Cresswell, 2000) anasema sampuli lengwa ndiyo iliyotumika katika kupata data katika tamthiliya mbili teule kwa sababu tunafahamu fika kwamba kutokana na sampuli hii tutafanikiwa kupata muafaka za kujibu maswali ya utafiti.

3.5 Vyanzo vya Data

Utafiti huu utakusanya data za msingi wa data za upili kama zinavyofafanuliwa hapa chini.

3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni halisi ambazo hazijawahi kukusanywa na mtafiti yeyote yule kwa madhumuni ya kuyajibu maswali ya utafiti yanayojibiwa katika utafiti huu ili kujaza pengo la utafiti ulioachwa na watafiti tangulizi (Kombo na Tromph, 2006). Data hizi zilikusanywa kutoka katika tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata* za Emmanuel Mbogo. Data hizi za msingi zitakusanywa katika machapisho mbalimbali ambayo yanahusiana na mada ya utafiti huu.

3.5.2 Data za Upili

Data za upili ni aina ya data za utafiti ambazo tayari zilikwishakukusanywa na watafiti watangulizi na kuchapishwa katika machapisho na maandiko mbalimbali (Yin, 1994). Data za upili hutumiwa katika utafiti kwa lengo la kujazilishia au kukazia maarifa mapya yletwayo na data za msingi za utafiti husika. Kothari (2004) anaiita mbinu hii kuwa ni mbinu ya kukusanya data za utafiti mezani ikiwa na maana

kuwa mtafiti haendi uwandani bali huenda katika maktaba na kuanza kukusanya data. Katika utafiti huu tumekusanya data za upili za utafiti wetu katika maktaba za Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Makavazi ya TATAKI na maktaba ya Mkoa wa Mwanza. Katika maktaba hizi tumesoma, tasinifu, vitabu, makala, majarida, tovuti na wavuti ili kupata data zilizohitajika katika utafiti wetu.

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kama inavyowasilishwa hapa chini.

3.6.1 Usomaji Makini

Usomaji makini humpa mtafiti fursa ya kusoma andiko husika kwa utulivu na umakini halafu akaweza kubaini data ambazo anazihitaji (Kombo na Tromph, 2006). Kothari (2008) anaelezea mbinu ya usomaji makini kuwa ni nzuri isiyopoteza muda katika ukusanyaji wa data. Anaendelea kueleza kuwa, usomaji makini ni mbinu ya haraka katika kukusanya data hasa pale mtafiti anaposoma andiko husika kwa utulivu na kulirudia mara kadhaa. Mbinu hii humpatia mtafiti data kirahisi na tena data ambazo ni mwafaka kwa ajili ya utafiti.

Pamoja na hayo mtafiti anahitajika kuandaa shajara pale anapoaanza kusoma kazi husika kwa ajili ya kudondolea data za utafiti. Kwa kutumia mbinu hii ya utafiti tulihakikisha tunaandaa shajara au daftari maalumu tulilolitumia katika kuhifadhi data za utafiti wetu. Ili kufanikisha hilo tulisoma tamthiliya moja baada ya nyingine na kila tulipobaini mbinu za tanzia za Ki-Aristotle, tulidondoa katika daftari letu. Kwa hiyo

daftari letu la kukusanyia data lilikuwa limegawanyika katika sehemu tatu: sehemu ya kwanza ilihusu mbinu za tanzia za Ki-Aristotle, sehemu ya pili ilihusu dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya husika na sehemu ya tatu ilihusu mbinu ambazo si za Ki-Aristotle katika tamthiliya husika.

3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data katika utafiti huu utafanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa maana ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti (Bagdan na Biklen 1992) kwa msingi huu tutaongozwa na na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo katika uchambuzi wa data za utafiti wetu. Mbinu hii humruhusu mtafiti kulisoma andiko fulani kwa ajili ya kulielewa katika maudhui, fani, falsafa na mengineyo. Baada ya kufahamu hayo, mtafiti atatumia njia ya maelezo isiyohusisha kanuni mbalimbali za kimahesabu katika kuzichambua data hizo na kuzifanya rahisi kueleweka kwa msomaji.

3.7.1 Mkabala wa Kidhamira

Utafiti huu umetumia mkabala wa kidhamira katika kuchambua data za utafiti wake. Aronson (1992) akiwanukuu Taylor na Broad (1984), Benner (1985) na Leininger (1985) anasema, mkabala wa kidhamira hutumika katika kuchambua kazi za kifasihi kwa kutumia hatua nne: Hatua ya kwanza kukusanya data, hatua ya pili ni kuoanisha data na mada ya utafiti, hatua ya tatu ni kupangilia data yaani kuoanisha dhamira kuu na dhamira ndogo, hatua ya nne ni kutoa maelezo juu ya data zilizokusanywa ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti husika.

Katika kufanikisha uchambuzi wa data za utafiti huu tumefanya uchambuzi kwa kutumia hatua zote nne. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kukusanya data za utafiti na hatua ya pili ikawa ni ni kuoanisha mada kuu na ndogondogo ambazo zimetumiwa katika uchambuzi wa data. Hatua ya tatu ilikuwa ni kupangilia data kwa kuweka pamoja zile zinazofanana na kuweka pembeni zile zisizofanana. Katika hatua ya nne, tumezitolea maelezo data tulizozikusanya kwa namna ambayo inajibu maswali yetu ya utafiti.

3.8 Usahihi wa Mbinu za Utafiti

Utafiti wa kisayansi au kitaaluma, humefanywa kwa kuzingatia mbinu mbalimbali zinazokubalika kuufanya kuwa ni utafiti usioeleza mambo ya ya uongo yasiyo na ukweli wa aina yoyote. Utafiti huu umetumia mbinu za uchambuzi wa kimaudhui mkabala wa kidhamira na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Nadharia ya Ki-Aristotle itaongoza utafiti huu katika hatua mbalimbali za uchambuzi wa data, Usahihi huu umejadiliwa katika mawasiliano ambayo wanafasihi wakiongozwa na Maprofesa waliohudhuria.

3.8.1 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huaminika pale ambapo taratibu zote za Utafiti zilizoainishwa katika Pendekezo la Utafiti lilitakalowasilishwa na kujadiliwa zimefuatwa kabla mwanafunzi hajaruhusiwa kukusanya data za utafiti wake, utafiti huu umefuata taratibu zote muhimu zinazotakiwa mpaka kufikia hatua hii, mbinu zote za utafiti pamoja na nadharia zimetumiwa kama inavyopaswa pale mtafiti alipopata ugumu alikwenda kwa msimamizi wake na kufanya mashauriano mbalimbali yaliyosaidia kukamilisha kazi hii ya utafiti.

3.8.2 Maadili ya Utafiti

Maadili ni dhana pana inayorejelea kuheshimu taratibu, miiko, mila na desturi mbalimbali katika jamii (Kumer 1999), Utafiti kama ilivyo katika mambo mbalimbali katika jamii, una miiko yake inayopaswa kuzingatiwa utafiti huu umefanywa kwa misingi kwamba miiko yote iliyojitokeza katika utafiti huu imefanywa kwa usahihi na kwamba yote yamedondolewa katika kazi zilizoteuliwa na si vinginevyo.

3.9 Hitimisho

Kimsingi sura hii imefafanua mambo kadhaa ambayo ni ya msingi kujadiliwa, hii ni pamoja na mbinu zilizomuongoza mtafiti kupata data, eneo la utafiti na namna ya uchambuzi wa data. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji uchambuzi wa data na mjadala unaotokana na ukusanyaji wa data mbalimbali zilizopatikana kutokana na utafiti huu.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii pamoja na sura zingine, inajaribu kuelezea kwa kina yale ambayo yamekuwa yakisemwa katika sura zilizotangulia kuhusu utafiti huu. Utafiti huu unalenga kuchunguza na kubainisha mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* na *Sundiata* ili kuona jinsi gani mbinu hizi zilivyotumika katika tamthiliya teuliwa ili kujibu maswali matatu ya misingi ambayo yameibuliwa katika sura ya kwanza kwa kuzingatia tafsiri za kiutamaduni.

Lengo kuu la sura hii ambayo inajibu swali la kwanza la utafiti huu ni kubainisha chunguza mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Pia swali la pili la utafiti huu ambalo ni kubainisha mbinu ambazo si za Ki-Aristotle zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*, ili kubaini ni mbinu zipi zilizotumiwa na msanii katika kujenga kazi zake za sanaa. Swali la tatu la utafiti huu ni kubainisha, kuelelezea na kujadili dhamira inayojibainisha katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Katika sura hii data zilizokusanywa katika utafiti huu, zimechambuliwa kwa kutumia kanuni na msingi wa nadharia ya Ki-Aristotle. Katika uchambuzi wa data za utafiti huu, ambazo zimepatikana kwa kutumia mbinu ya maktaba.

4.2 Mbinu za Tanzia za Ki-Aristotle, Zisizo za Ki-Aristotle na Dhamira katika Tamthiliya ya Fumo Liongo

Katika sehemu hii, mtafiti amejibu swali la kwanza la utafiti ambalo ni; mbinu zipi za tanzia za Ki-Aristotle zilizotumika katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*, mtafiti

amechunguza pia mbinu za kifani ambazo zimetumika katika kutunga tamthiliya ya *Fumo Liongo*, mtafiti aligundua kuwa utunzi wa tamthiliya hii umejikita katika misingi ya Ki-Aristotle. Kwa hiyo basi, utafiti huu ulijaribu kuchunguza mbinu za tanzia za Ki-Aristotle kama zilivyotumika katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*.

Kwa mujibu wa Aristotle tamthiliya yoyote kwa kawaida ina vipengele vifuatavyo:-

(1) Msuko, (2) Wahusika, (3) Dhamira, (4) Uteuzi wa matumizi ya maneno,
(5) Nyimbo, (6) Maonesho. Pia aliugawa mchezo wa kuigiza katika sehemu tatu: Sehemu ya kwanza ni ile ya mwanzo, au tangulizi, Sehemu ya pili ni ya kitendo chenyewe, Sehemu ya tatu ni wimbo, ili aweze kuwasiliana na hadhira yake juu ya ujumbe, msimamo na falsafa ya maisha.

4.2.1 Mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika Tamthiliya ya Fumo Liongo

4.2.1.1 Msuko

Katika utafiti huu, mtafiti amegundua kuwa mtiririko wa vitendo katika tamthiliya ya Fumo Liongo umepangwa kufikia kilele. Kama katika tamthiliya za Aristotle, mpangilio huu humpatia mtazamaji huruma na hofu. Kitendo cha pili hutokana na kusababishwa na kitendo cha kwanza, kwa mfano katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*, matukio yamepangwa katika matendo matano ambayo yanatendwa na wahusika yakiendana na tabia na matendo yao. Mwandishi anayadhihirisha haya kupitia Mfalme Daudi Mringwari Mfalme wa Pate ambaye tabia yake ni ukatili na matendo yake ni ya udhalimu. Anamuua Msheki Waziri wake kwa kuwa anapingana naye (Uk. 7), Mandhari ni ya Kiafrika ili kuifahamisha jamii ya Kiafrika kwa ujumla juu ya athari za watawala dhalimu na madikteta katika jamii za Kiafrika. (Semzaba 1997), na Mulokozi (1996).

4.2.2 Wahusika

Kwa mujibu wa Semzaba (1997:76), tamthiliya hutawaliwa na migongano ambayo huwekwa wazi, hukuzwa na kusuluhishwa. Migongano hii hupewa wahusika ambao kwa matendo na maneno huwakilisha kwa hadhira kutokana na falsafa ya jamii au ya mwandishi mwenyewe. Wahusika wanapambanishwa na kugawanywa katika pande mbili tofauti: Upande unaokubalika na jamii kuwa ndio wenye maadili bora, upande mwingine ni ule uliokinyume na maadili bora ya jamii. Katika tamthiliya ya Fumo Liongo, mtafiti amegundua kuwa upande wa *Fumo Liongo* ndio unaokubalika na jamii kuwa wenye maadili bora. Umepambanishwa na upande wa Mfalme Daudi Mringwari ambapo upo kinyume na maadili bora ya jamii.

Kwa matumizi yamaneno katika kitendo cha kwanza (Uk 4-7), mwandishi anauweka wazi mgongano uliopo ambao ni wa Kisiasa, Kiutamaduni na Kiuchumi. Kitendo cha tatu (Uk 24), hadi kitendo cha tano (Uk 36), mwandishi anaukuza mgongano uliopo katika Kaditama (Uk 49), mwandishi anausuluhisha mgongano uliopo. Mwandishi katika Kaditama anaonesha falsafa yake kuhusu siasa ya kwamba siasa mbovu za ukandamizaji hazikubaliki na jamii.

4.2.3 Dhamira

Dhamira katika utunzi ni nyingi kama vile:-Dhamira ya Ukombozi: ukombozi wa Wanawake, Ukoloni na Ukoloni mamboleo. Kila dhamira ina uzito kama jambo ambalo linachangia maendeleo ya jamii. Dhamira zingine ni kama vile: Mapenzi, Urithi, Ushujaa, Wivu na Rushwa. Dhamira hizi uweza kutumiwa na mtunzi kuongelea kuhusu Ukoloni mamboleo au Ukombozi kwa kujiweka salama kutokana na tabaka tawala (Semzaba 1997). Katika utafiti huu, mtafiti amegundua dhamira ya

Ukombozi kuhusu ukoloni mamboleo, amegundua pia kwamba, mwandishi ametumia dhamira zingine kama: Rushwa, Mapenzi, Ushujaa na Usaliti kulikosoa tabaka tawala.

4.2.4 Fikra

Kwa mujibu wa Aristotle (1958), fikra ni matokeo ya utumiaji wa lugha katika tamthiliya, mara nyingi fikra ni sehemu ya matamshi (Hussein, 1983:204). Lugha ni muhimu kwani hupitisha ujumbe wa mtunzi kwa hadhira kupitia wahusika. Lugha ya tamthiliya ni rasmi na ya mkato inayoonesha mgongano katika jamii na usuruhishi wake kwa muda mfupi kwa kuwa kila neno lililoandikwa huchangia jambo muhimu katika tamthiliya. Kama mtunzi ana lengo la kulikosoa tabaka tawala au taasisi zenye nguvu zisizokubali kukosolewa bila kutumia mabavu, bora kutumia lugha nzito zenye mafumbo. Lugha ya picha na tamathali za semi ili kumuweka mtunzi salama na hofu hii.

Pamoja na matumizi ya lugha, nyimbo, muziki na ngoma hutumika kupeleka ujumbe kwa hadhira. Pia utunzi wa fani za sanaa za asili za Kiafrika husaidia ujumbe kueleweka vema miongoni mwa adhira ya Kiafirka (Semzaba, 1997:78) Katika utafiti huu, katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* mtafiti amegundua kuwa mwandishi ametumia lugha rasmi na ya mkato kupitisha ujumbe wake kwa hadhira kupitia wahusika. Yapo pia matumizi ya nyimbo (Uk 25), matumizi ya ushairi wa kisasa (Uk 49-51), matumizi ya ngoma (Uk 9-10).

Mtafiti amegundua pia kwamba kuna matumizi ya mafumbo mfano, mafumbo yenye mafundo au mafundo yenye mafumbo (Uk 6). Mwandishi ametumia tamathali za

semi, mfano, miguu miwili iendayo uchiuchi (Uk 1) – Tashihisi. Kama jinga la moto katikati nyasi kavu za Wabajui (Uk 4), Tashibiha. Joka hili mahsusi sasa latemea na kumezea mate kiti cha enzi ya Ufalme wa Pate (Uk 78) – Taswira. Kuchonga mdomo (Uk 14,15) – Msemo. Liongo! Simba! Liongo! Simba! (Uk 1) – Takriri.

4.2.5 Mtungo wa Tamthiliya

Semzaba (1997), akimuunga mkono na Hussein (1983), anasema umbo la Tanzia ya Ki-Aristotle ni umbo lenye mtungo mzuri uliokuwa na mwanzo, kati, na mwisho na utawaliwa na migongano. Katika sehemu hizo tatu, huna budi kuweka wazi mgongano uliopo, kuukuza na kuusuluhisha. Katika utafiti huu mtafiti amegundua kuwa mwandishi wa tamthiliya ya *Fumo Liongo* ameugawa mchezo wake katika sehemu tatu kulingana na mtiririko wa matukio katika vitendo.

Tamthiliya ya *Fumo Liongo* imegawanyika katika vitendo vitano: Kitendo cha kwanza na cha pili mwandishi anauweka wazi mgongano uliopo kati ya pande mbili tofauti za wahusika, upande wa Fumo Liongo aliyekuwa maarufu na kupendwa na watu kwa ajili ya ushujaa vitani, Malenga stadi na mkosoaji wa siasa za Sultani (Uk 4) katika kitendo cha tatu mwandishi anaukuza na kuufikisha mgongano kileleni. Kitendo cha nne hadi cha tano mwandishi anausuluhisha mgongano kwa kifo cha Fumo Liongo.

4.3 Mbinu zisizo za Ki-Aristotle Katika Tamthiliya ya Fumo Liongo

Katika sehemu hii, mtafiti anajibu swali la pili la utafiti linalouliza kwamba: ni mbinu zipi zisizo za Ki-Aristotle zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*.utafiti wetu umegundua kuwa mbinu hizo ni Utendi, Majigambo,

kuchanganya Ushairi na Nathari zilizochotwa kutokana na sanaa za Jadi za Kiafrika ili kuwa na tamthiliya za Kiafrika (Mulokozi 1996:210). Utafiti huu umegundua kuwa kuna mbinu zisizo za Ki-Aristotle kama vile kuchanganya tanzia na ufutuhi, Miungu kutokuwa na kauli.

4.3.1 Mbinu za Utendi

Ni moja ya mbinu hii inatumia mbinu ya Usimulizi, Diolojia na Utendaji, mbinu hii hutumiwa ili kusadifu malengo yake. Katika utafiti wa tamthiliya ya *Fumo Liongo*, mtafiti amegundua kuwa mwandishi ametumia mbinu ya utendi kama kuipa umbo tamthiliya yake.

4.3.1.1 Mbinu ya Usimuliaji

Mutembei (2010), anasema, usimuliaji ni namna mtunzi anavyotoa visa vyake kupitia kwa wahusika ambao anawapa lugha, matendo na kuwavisha uhalisia kuna matumizi ya Korasi katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*

4.3.1.2 Mbinu ya Diolojia

Haya ni mazungumzo ya wahusika katika tamthiliya. Dialojia huwa na maneno machache yaliyoteuliwa vizuri ili kuisogeza mbele hadith au kudhihirisha jambo fulani alilokusudia mtunzi. Mbinu hii hutumika katika drama na tendi. Utafiti huu uligundua matumizi ya mbinu ya dialojia katika tamthiliya ya Fumo Liongo kwa mfano kuna majibizano (Uk 16).

LIONGO: Karibu Mwanangu

ZAHIDI: Asante.

4.3.1.3 Mbinu ya Monolojia

Monolojia ni usemaji nafsi au usimulizi mfano, katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* Machaka anasimulia njama ya kumuangamiza Liongo zinazopangwa na Maringwari na Waziri kiongozi ili kuuzima umaarufu wake. (Uk 11).

4.3.2 Mbinu ya Majigambo

Majigambo ni mbinu ya kisanaa ya kusimulia kwa kujinadi au kujikweza kwa mtu/kitu kuhusu matendo na mambo muhimu ya kishujaa na kishupavu aliyoyafanya kwa uwezo wake au kwa nasaba yake. Katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*, mwandishi ametumia mbinu ya majigambo kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Mwandishi amempa lugha ya majigambo mhusika wake ili kuelezea hali halisi ya jamii yenye matabaka, Tabaka tawala lenye uwezo na nguvu na Tabaka tawaliwa la chini. Hali hii inaoneshwa na mhusika Mringwari anaposema:

> **MRINGWARI:** Na kama hujui, hutalijia asilani!
>
> Mjinga mkubwa we! Punde si punde nitakuonyesha kuwa katika nchi hii ya Pate ni mimi tu. Ninayeweza kuchezea na kupitua pitua solo za ufu na uhai wa Wabajuni (Uk 6)

4.3.3 Mbinu ya Kuchanganya Ushairi na Nathari

4.3.3.1 Utangulizi

Utafiti huu unalenga kubainisha dhamira zinazoibuliwa na mbinu za Ki-Aristotle. Lengo hili linahusika na ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu fani na maudhui (dhamira) haviwezi kutenganishwa. Ushairi ni sanaa inayotumia lugha ya mkato ilihali nathari inatumia lugha isiyo ya mkato. Mbinu hii imetumiwa na mtunzi wa tamthiliya ili kupamba kazi yake ya sanaa na kuwasilisha mahudhui yake.

Mfano, shairi linaloonekana katika sehemu ya Kaditama linaonyesha nguvu za tabaka tawala, pia linaonyesha mwanzo wa mapambano ya ukandamizwaji unaofanywa na tabaka tawala. Tamthiliya hii imeandikwa pia kinathari kwa kuandika sentensi ndefu. Mbinu hii ya kuchanganya ushairi na nathari inaonyesha mchanganyiko wa tamaduni mbili ya asilia na ya kigeni.

4.4 Maudhui katika Tamthiliya ya Fumo Liongo

Katika kujibu swali la tatu la utafiti wetu, utafiti huu ulichunguza kwanza maudhui yanayojitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Mtafiti alibainisha dhamira kwa kutumia mbinu ya maelezo. Dhamira zilizobainishwa ni (i) Uongozi kandamizi, (ii) Rushwa, (iii) Usaliti, (iv) Matabaka (v) Nafasi ya Mwanamke katika Harakati za Ukombozi.

4.4.1 Uongozi Kandamizi

Utafiti kuwa huu, uligundua kuwa mwandishi amemsawiri Daudi Mringwari kama kiongozi anayetawala kwa Imla na Hofu iliyotokana na umaarufu wa *Fumo Liongo* nduguye, shujaa vitani, aliyependwa na watu, Malenga Stadi na mkosoaji wa siasa za Sultani Daudi Mringwari. Kila aliyesema ukweli kuhusu Fumo Liongo, Mringwari alimuangamiza mfano mzuri uko (Uk 7).

MRINGWARI: Huyo! Mtalimbo toka utosini
Kisha mtoseni baharini
Haya yanadhihirishwa na Mbwasho kuwa Msheki
kauwawa na mazabania.

MBWASHO: Kawaje! Mnaleta mchezo sana nyie.
Msheki kauchonga mdomo Mringwari kaula kaushiba
Leo mazabania wa Ikulu wamemuua (Uk 15).

4.4.2 Rushwa

Utajiri na nguvu za dola zinatumika kumnunua na kumlaghai Zahidi ambaye hatimaye anatumwa kwenda: (a) Kuipeleleza siri ya uhai wa na ufu wa Fumo Liongo (b) Kumuuwa Liongo msituni kwa sindano ya shaba. Haya yanadhihirishwa kupitia kwa mhusika Mringwari anaposema.

MRINGWARI: Wazo lako zuri sana. Yaani tumpate mtu ndugu ama rafiki, kisha tumnunue kwa pesa nyingi (Uk 31)

Pia mhusika W. Kiongozi anadokeza hili:

MBWASHO: Mtukufu Mfalme, ahadi za mali, vyeo na unyumba unaomsubira Zahidi baada ya kuibukkua siri ya uhai wa Fumo Liongo ni ulimbo uwezao kumnasa hata tai, Sembuse yule njiwa dhaifu arukae kufuata upepo (Uk 36).

4.4.3 Usaliti

Utafiti huu ulibaini kuwa katika tamthiliya hii ya Fumo Liongo, yupo msaliti mmoja ambaye ni Zahidi mtoto wa kufikia wa Fumo Liongo. Lakini anakubali kununuliwa na kumuua baba yake aliyemlea. Haya yanadhihirishwa na Fumo Liongo anapolia hivi:

LIONGO: Zahidi mwanangu umeniua?

Kakununua Mringwari! Umenunulika?

4.4.4 Matabaka

Utafiti huu ulibaini kuwa katika tamthiliya hii kuna matabaka, tabaka la mabwana na tabaka la wajakazi, haya yanaonyeshwa na Liongo (Uk 25) pia katika wimbo anaoimba Sada (Uk 25).

4.4.5 Nafasi ya Mwanamke katika Harakati za Ukombozi

Waandishi mbalimbali wa fasihi wanachora wanawake katika nafasi mbalimbali kwa mfano katika utafiti huu, mtafiti amegundua kuwa mwandishi amemchora mwanamka kama jasiri anayejitoa mhanga katika ukombozi, anamtumia Sada kijakazi wa Fumo Liongo ambaye anafanikiwa kumtoa Liongo gerezani kwa kumpelekea mkate wenye tupa, pia kamba ambazo alivitumia Liongo kutoroka gerezani (Uk 26).

4.5 Hitimisho

Sehemu hii imejadili kwa kina mbinu za tanzia za Ki-Aristotle na mbinu ambazo si za Ki-Aristotle. Vilevile, sura hii imejadili maudhui yaliyojitokeza katika tamthiliya ya *Fumo Liongo*. Utafiti huu umegundua kwamba, tamthiliya hii ni ya kisasa ambayo imetumia mbinu ya Ki-Aristotle katika muundo wake pia ametumia mbinu nyingine ambazo si za Ki-Aristotle kuonyesha matokeo ya tamaduni mbili ya kigeni na ya asili na amejenga ujumi wa kimseto.

4.6 Mbinu za Tanzia za Ki-Aristotle, zisizo za Ki-Aristotle na Dhamira katika Tamthiliya ya Sundiata

Lengo kuu ya sehemu hii, ambayo inajibu swali la kwanza la Utafiti huu ni kuibua, kuelezea na kujadili mbinu za Ki-Aristotle zinavyojitokeza katika tamthiliya ya *Sundiata* ili kuona ni mbinu zipi za tanzia za Ki-Aristotle zilizotumika kujenga kazi hii ya sanaa. Katika sura hii data zilizokusanywa zimechambuliwa na kujadiliwa kwa kutumia kanuni na misingi ya Ki-Aristotle. Pia nadharia hii ilitumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu ambazo zilipatikana kwa kutumia mbinu ya maktaba. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu ya maktaba kuchunguza mbinu

za tanzia za Ki-Aristotle na zile ambazo si za Ki-Aristotle zilivyojitokeza katika tamthiliya ya *Sundiata*.

4.6.1 Mbinu za Ki-Aristotle katika Tamthiliya ya Sundiata

Utafiti huu, ulihchunguza mbinu za kifani ambazo zimetumika kujenga tamthiliya ya Sundiata, utafiti huu uligundua kuwa ujenzi wa tamthila ya *Sundiata* umo katika misingi ya Ki-Aristotle. Kwa hiyo basi, utafiti huu ulijaribu kuchunguza mbinu za tanzia za Ki-Aristotle zinavyojitokeza katika tamthiliya ya Sundiata. Kwa mujibu wa Aristotle tamthiliya yoyote kwa kawaida huwa na vipengele vifuatavyo: (i) Msuko, (ii) Wahusika, (iii) Dhamira, (iv) Uteuzi wa matumizi ya maneno, (v) Nyimba, (v) Maonesho.

4.6.1.1 Msuko

Msuko ni mpangilio wa visa na matukio katika kazi ya fasihi. Katika utafiti huu, mtafiti amegundua kuwa tamthiliya ya *Sundiata* imejengwa katika mtiririko wa vitendo vitano, vilivyopangwa ili kufikia kilele. Mpangilio huu humpatia mtazamaji huruma na hofu. Mpangilio huu wa vitendo umepangwa ili kitendo cha kwanza kitokane na kusababishwa na kitendo cha pili. Msuko huu wa matukio umepangwa ili kuonyesha mgongano mkubwa wa madalaka, unaochukua pande mbili, zikiwa na funzo kwa jamii husika. Mgongano huu uendelezwa hadi suluhisho kulingana na falsafa ya mwandishi.

4.6.1.2 Wahusika

Wahusika ni watu au vitu vinavyowasilisha wahusika wa kazi za fasihi ambayo huibua migongano mbalimbali katika kazi za fasihi. Tamthiliya hutawaliwa na

migongano ambayo upewa wahusika wanaopambanishwa na kugawanywa katika pande mbili tofauti kwa matumizi ya matendo na maneno. Migongano hiyo huwekwa wazi mwanzoni mwa tamthiliya undedelezwa katika sehemu ya kati na husuruhishwa mwishoni (Semzaba 1997).

Katika tamthiliya ya *Sundiata* wahusika wamegonganishwa katika pande mbili tofauti, upande unaokubalika na jamii kuwa wenye maadili bora unajumlisha wahusika kama: Sundiata, Sogoloni, Balla Fasseke na Nana. Upande ulio kinyume na maadili bora ya jamii, kulingana na falsafa ya jamii au ya mwandishu unajumlisha wahusika kama: Sassuma, Dankarani, Waziri Sumaguru. Kwa matumizi ya maneno na matendo mwandishi ameuweka wazi mgongano katika Machweo na katika kitendo cha kwanza mgongano huu ni wa kuwania madaraka (Uk xvii – 21). Kitendo cha pili hadi cha tatu umekuzwa na umesuruhishwa katika kitendo cha nne na cha tano.

4.6.1.3 Dhamira

Dhamira ni wazo ambalo mwandishi anataka kulitoa kwa hadhira yake. Katika utunzi wa tamthiliya kuna dhamira nyingi kama vile Ukombozi wa mwanamke, Ukoloni, na Ukoloni Mamboleo. Dhamira zingine ni Mapenzi, Urithi, Ushujaa, Rushwa na Wivu. Dhamira hizi huweza kutumiwa na mtunzi kuongelea kuhusu ukoloni mamboleo ili mwandishi ajiweke salama kutokana na tabaka tawala (Semzaba (1997). Utafiti huu umegundua kuwa dhamira kuu ni urithi. Pia kuna dhamira zingine kama Rushwa, Ushujaa, Mapenzi nakadharika. Katika tamthiliya ya *Sundiata* ambazo mwandishi amezitumia ili kulikosoa tabaka tawala katika bara la Afrika na kwingineko duniani.

4.6.1.4 Fikra

Ni matokeo ya matumizi ya lugha katika tamthiliya na mara mara nyingi ni sehemu ya matamshi (Hussein 1983). Lugha ni muhimu kwa kupitishia ujumbe wa mwandishi kwa hadhira kupitia kwa wahusika. Lugha ya tamthiliya ni rasmi na ya mkato inayoonyesha migongano katika jamii na usuruhishi wake kwa muda mfupi.

Katika utafiti huu wa tamthiliya ya *Sundiata* mtafiti amegundua kuwa lugha ni ya mkato na rasmi, matumizi ya nyimbo (Uk 29-34), tamathali za semi mfano, tashihisi: Si haki kiendelee kupgwa baridi kwa utupu hali kikililia joto la makalio ya ufalme (Uk 2), kejeli :Ee! Cheka we Sassuma! Ishi! (Uk 7), pamoja na hayo kuna matumizi ya mashairi ya kisasa (Uk xvii), ushairi huu unaweka wazi tatizo. Kuna pia matumizi ya mazungumzo ya kitamthiliya ambayo yanaonyesha hali ya mchezo mfano;

NANA: Kauli ya baba

SASSUMA: Wewe! (Uk 5). Haya ni maneno machache yaliyotumiw na mtunzi ili kutupa habari kuwa kuna jambo litatokea jambo hilo ni la kuwania madaraka

4.6.1.5 Mtungo wa Tamthiliya

Umbo la tanzia ya tanzia ya Ki-Aristotle ni yenye mtungo mzuri wenye Mwanzo, Kati na Mwisho unaotawaliwa na migongano sehemu ya mwanzo ni ya kuuweka wazi mgongano uliopo sehemu ya kati ya kuukuza na kuuendeleza na sehemu ya tatu ni ya kuusuruhisha (Semzaba 1997), (Hussein, 1983). Katika utafiti wa tamthiliya ya *Sundiata* mtafiti amebaini kuwa, mwandishi ameugawa mchezo katika vitendo vitano, vitendo hivi vimepangwa katika sehemu tatu kama ifuatavyo:

Kitendo cha kwanza na cha pili mgongano umewekwa wazi (Uk. 1-31). Kitendo cha tatu na cha nne mgongano umekuzwa na kuendelezwa hadi kilele (Uk. 34-66). Kitendo cha tano mgongano una suruhishwa kwa kifo cha Sundiata (Uk. 70-72). Mwandishi amegundua pia kwamba sanaa ilishikiriwa na tabaka tawala lililojiweza ambalo lilifanya fani isimamie matakwa yake. Hii ndio falsafa ya mwandishi kuhusu madaraka.

4.6.2 Mbinu Sisizo za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya Sundiata

Utafiti huu unajibu swali la pili la utafiti lililouliza: Ni mbinu zipi zisizo za Ki-Aristotle zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Sundiata?* Mbinu hizo ni: (i) Mbinu za utendi, (ii) Mbinu ya Majigambo, (iii) Mbinu ya Uchawi, na Uganga, (iv) Mbinu ya Nyimbo na Ngoma, (v) Mbinu ya kuchanganya Ushairi na Nathari. Mbinu hizi zimechotwa kutokana na sanaa za jadi za Kiafrika ili kuwa na tamthiliya za Kiafrika (Mulokozi 1996).

4.6.2.1 Mbinu ya Utendi

Mbinu ya utendi inatumia mbinu ya usimuliaji, Dialojia na Utendi mbinu hii ilisadifu malengo yake. Utafiti wa tamthiliya ya *Sundiata* umegundua kuwa Mwandishi ametumia mbinu ya utendi kama kielelezo cha ubatili wa kuwania mamlaka (Mulokozi, 2011).

4.6.2.2 Mbinu ya Usimuliaji

Usimuliaji ni namna mtunzi anavyotoa visa vyake kupitia kwa wahusika ambao anawapa lugha, matendo na kuwavika ualisia, pia mwandishi hutumia Dialojia

(Majibizano) ili kufikisha ujumbe wake kwa hadhira (Mtembei 2010), katika utafiti wa tamthiliya hii mwandishi ametumia mbinu hii ili kufikisha ujumbe kwa hadhira.

4.6.2.3 Mbinu ya Dialojia

Haya ni mazungumzo ya wahusika katika tamthiliya yenye maneno machache yaliyoteuliwa vizuri kuusogeza mbele mchezo, hadithi au kudhihirisha jambo fulani alilokusudia mtunzi mbinu hii hutumika katika drama – tendi: Utafiti huu uligundua matumizi ya dialojia katika tamthiliya ya Sundiata mfano,

MAGWILA: Sasa mkate shingo!

KONKOMBA: Mkate shingo asidi! (Uk. 14)

4.6.2.4 Mbinu ya Monolojia

Monolojia ni usemaji nafsi au simulizi, mfano katika tamthiliyaya Sundiata, Morani 2, anasimulia hadithi kuhusu vita katika kitendo cha pili huko Mema ukiongozwa na jemedali Sundiata mwana wa Sogoloni (Uk. 36).

4.6.2.5 Mbinu ya Majigambo

Majigambo ni mbinu ya kusimulia kwa kujidai au kujikweza kwa mtu au kitu kuhusu matendo na mambo muhimu ya kishujaa na kishupavu aliyoyayafanya kwa uwezo wake au kwa nasaba yafanya kwa uwezo wake au kwa nasaba yake (Mulokozi, 1996). Utafiti huu umegundua kuwa, mwandishi ametumia mbinu ya majigambo, kwa kuwapa lugha ya majigambo wahusika Konkomba na Magwila wajinadi na kujikweza kuhusu uwezo wao wa kichawi (Uk. 30).

KONKOMBA: Tumefika shetani wa mauti!

MAGWILA: Tumefika wachimbua mauti!

KONKOMBA: Tumefika wapanda fisi usiku!

Kwa hiyo mwandishi ametumia lugha ya majigambo kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira ili kuelezea hali harisi ya matumizi ya uchawi kama njia ya kumwezesha Dankarani akalie kiti cha Ufalme kinyume na matakwa ya baba yake aliye amini utabiri wa Miungu ya Wamandingo.

4.6.2.6 Mbinu ya Kuchanganya Ushairi na Nathari

Utafiti huu umegundua kuwa mwandishi amechanganya ushairi na nathari ili kuipamba kazi yake ya sanaa na kuwasilisha maudhui yake mfano, ushairi katika Machweo (Uk. xvii) umeweka wazi mgongano mkubwa wa madaraka ambao unachukua pande mbili. Mwandishi ametumia lugha ya kinathari ili kuelezea maudhui yake kwa urahisi na kwa ufupi. Vilevile mbinu hii inaonyesha kuwa tamthiliya hii ya majaribio inayotumia vipengele vya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.

4.6.2.7 Mbinu ya Uchawi na Uganga

Ni mbinu ambayo utafiti umebaini katika tamthiliya ya *Sundiata*. Mwandishi ametumia mbinu ya uchawi ili kuonyesha hadhira ujanja wa tabaka tawala katika kuhakikisha wanabaki madarakani muda wote bila kujali jinsi wanavyotawala. Tabaka hili huwatisha watu wa tabaka tawaliwa ili waendelee kuamini kwamba viongozi wao wanauwezo mkubwa ambao hauwezi kuhojiwa na mtu yeeyote na kwamba wao lazima wachukuliwe kuwa ni viongozi wa maisha. Mfano (Uk. 60) Sumanguru anaongea:

SUMANGURU: Ninazo, lakini yeye na Sundiata watajutia siku walipotanguliza

Vichwa.

Katikati ya mapaja ya mama zao,

Yaliyotetemeka kwa matungu,

Ili kuingia hii chungu. Niletee Bundi wangu (anamleta Bundi) Mbinu nyingine ambayo mwandishi ameitumia ni mbinu ya uganga kwa mfano, katika tamthiliya ya Sundiata (Uk 8-9) uganga anaofanyiwa Sundiata na Kolonkani kupitia matambiko ya Miungu wa Mandingo uliweza kumuondolea Sundiata ukiwete aliokuwanao, mbinu hii ni mbinu ya ukombozi.

4.6.2.8 Mbinu ya Nyimbo na Ngoma

Ngoma na nyimbo ni moja ya vipengele vya sanaa za maonesho za jadi za Kiafrika hutumika katika kuwasilisha ujumbe katika jamii. Mbinu hizi zimetumika pia katika tamthiliya ya *Sundiata* kama kibebaji cha ujumbe, Mfano (Uk. 8) ngoma imetumika katika kutangaza jina la Mfalme atakayetawala ambaye ni Dankarani pia mbinu hii imetumika ya ngoma imetumika pamoja na mbinu ya nyimbo (Uk. 21, 33, 42, 56), kuonyesha mtiririko wa matukio kutoka katika kitendo cha kwanza hadi kitendo cha mwisho.

4.6.3 Dhamira katika Tamthiliya ya Sundiata

Katika kujibu swali la tatu la utafiti wetu linalouliza: Ni maudhui yapi yanayojitokeza katika tamthiliya ya *Sundiata?* Utafiti huu ulichunguza kwanza

maudhui yanayojitokeza katika tamthiliya ya *Sundiata.* Mtafiti alibaini dhamira zifuatazo kwa kutumia mbinu ya maelezo: (i) Uongozi mbaya (ii) Rushwa (iii) Ushirikina (v) Nafasi ya Mwanamke katika Jamii.

4.6.3.1 Uongozi Mbaya

Utafiti huu umegundua dhamira ya uongozi mbaya katika tamthiliya ya *Sundiata*. Mwandishi anamwonyesha Sumanguru kuwa na hali zote za ukatili, udhalimu na ufisadi pamoja na udikteta, anasema kwa niaba ya watu. Anauwa watu ovyo pale wanapotaka kumpinga. Watu wake hawana uhuru wana mwabudu yeye kama Mungu. Ni mtawala asiyetaka mabadiliko, anataka kuendelea kutawala kwa ukatili, vitisho visivyo kifani pamoja na uchawi uliokithiri (Uk. 70-71).

4.6.3.2 Rushwa

Rushwa ni adui wa haki. Utafiti umebaini rushwa katika tamthiliya ya *Sundiata* ambayo imeonyeshwa (Uk. 21). Sassuma anamtoa Nana binti yake kwa Sumangulu ili kumtaka suluhu.

4.6.3.3 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Waandishi wengi wa tamthiliya huwachora wanawake katika nafasi mbalimbali kama vile, ulezi, huruma na ujasiri. Katika utafiti huu mtafiti amegundua kuwa mwandishi wa tamthiliya ya Sundiata amemchora mwanamke katika nafasi zifuatazo: (i) mwanamke kama mzazi (Uk. 34, 37), (ii) pia mwanamke amechorwa kama katili mfano Sassuma anamuuwa *Sundiata* na Nana kwa kuwachoma kisu (Uk. 74).

SASSUMA: Na wewe mbegu haramu, kufa umfuate kiwete kuzimu

NANA: (kwa uchungu) Aaa? Mama umeniuwa.

(anaanguka anakufa)

SUNDIATA: Sa-ssu-ma (anaanguka anakufa)

Mwanamke pia amechora kama mchawi (Uk. 11)

SASSUMA: Nimekwisha tuma ujumbe kwa Gwiji

Mama kokomba,

Atakuja punde

Viziba vya makalio, nywele

Na kipande cha nguo vipotayari

Hivyo mauti ya hasidi hayako mbali.

Haya yametiliwa mkazo kuwa, suluhisho la matatizo yote katika jamii zetu ni kupenda ukweli, kwani kufanya hivyo tunaepukana na jamii zenye matabaka yanayohasimiana na kusababisha migogoro ya kila aina inayokwamisha maendeleo ya jamii katika nyanja mbalimbali.

4.6.3.4 Ushirikina

Katika utafiti huu, mtafiti amebaini ushirikina katika tamthiliya ya *Sundiata*. Mwandishi anaonyesha ushirikina unaotumiwa na Sumangulu ili kuwafanya wale anaowatawala wakubaliane na anachokitaka (Uk. 58, 68) kama anavyosema Balla.

BALLA (ANATOA PEMBE): Mzizi wa ulozo wake ni huu

NANA: Ndio huu, kakaangu. Lakini kuna siri kubwa zaidi inayohusu makago ya mwili na ngome yake (Uk. 68)

4.7 Hitimisho

Sehemu hii imejadili mbinu za tanzia za Ki-Aristotle katika tamthiliya ya *Sundiata* mbinu hizo ni (i) Msuko (ii) Wahusika (iii) Dhamira (iv) Utenzi na matumizi ya maneno (v) Nyimbo (vi) Maonesho pia mchezo uligawanywa katika sehemu tatu: Mwanzo, kati na mwisho. Sehemu hii pia imejadili mbinu ambazo si za Ki-Aristotle ambazo ni: (i) Utendi (ii) Majigambo (iii) Ushairi na Nathari (v) Uchawi na Uganga (v) Nyimbo na Ngoma.

Vile vile, sehemu hii imejadili kwa kina dhamira yaliyojenwa kwa dhamira zifuatazo: (i) Uongozi mbaya, (ii) Rushwa, (iii) Nafasi ya mwanamke katika jamii. Pamoja na hayo mwandishi ameweza kujitambulisha vyema kwa utunzi wake katika upekee wa kazi zake za sanaa kwa kutumia vyema mbinu za Ki-Aristotle na zile ambazo si za Ki-Aristotle na hivyo kujenga ujumi mseto wa tamaduni mbili ule wa asili na ule wa kigeni na kuzifanya tamthiliya zake ziwe tamthiliya za tanzia za kisasa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Hii ni sura inayotoa muhtasali, tamati na mapendekezo kwa ajili ya utafiti zaidi hapo baadae. Katika kufanya hivyo, sura hii inagusia kwa ufupi yale yaliyowasilishwa, kuchambuliwa katika utafiti huu kwa ujumla wake. Kwa kuisoma sura hii, msomaji anaweza kupata picha ya matokeo ya utafiti kabla ya kusoma tasinifu hii yote.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo yamekamilika na hivyo kufanya lengo kuu la utafiti kutimizwa. Muhtasari wa kila lengo mahususi la utafiti huu ni kama ifuatavyo.

5.2.2 Mbinu za Ki-Aristotle katika Tamthiliya Teule

Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata* zinatumia mbinu za Kiaristotle katika kuwasilisha dhamira zake kwa wasomaji. Mbinu hizo ni pamoja na mtungo wa tamthiliya, utumiaji wa jukwaa, fikra, dhamira, wahusika na msuko. Mwandishi Emmanuel Mbogo ametumia mbinu hizi na kuzifanya kazi zake hizo mbili kuwa zenye kuvutia na rahisi kueleweka kwa wasomaji wake. Matumizi ya mbinu za Kiaristotle katika tamthiliya hizi mbili yanafanana bila kutofautiana hata kidogo jambo linaloonesha kuwa huu ndio mtindo wa mwandishi huyu katika utunzi wake wa tamthiliya. Hata hivyo, mtindo wa utunzi wa tamthiliya kwa mbinu za Kiaristotle unaelezwa na baadhi ya wataalamu kuwa ni wa kimagharibi zaidi na ndipo baadhi yao wakiongozwa na Ebrahim Hussein wakaja

na utunzi mpya wa tamthiliya. Utunzi huo ni ule wa kutumia mbinu za kijadi katika utunzi wa tamthiliya.

5.2.3 Mbinu Sizizo za Ki-Aristotle

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mwandishi Emmanuel Mbogo amefanikiwa si katika kutumia mbinu za Kiaristotle pekee bali hata mbinu nyingine zikiwemo za kijadi zinazotumiwa na akina Ebrahim Hussein, Penina Mlama na watunzi wengine. Mbinu hizo zisizo za Kiaristotle ambazo zinajitokeza katika *Fumo Liongo* ni kuchanganya mashairi na nathari, majigambo, monolojia, diolojia, usimuliaji, na utendi. Kwa upande wa tamthiliya ya Sundiata mbinu zisizo za Kiaristotle ni nyimbo na ngoma, ushairi na nathari, uchawi na uganga, mbinu ya majigambo, monolojia, diolojia, usimuliaji na utendi. Tunapozitazama mbinu hizi kwa makini tunabaini kuwa zinafafana na zinajitokeza hivyo hivyo katika tamthiliya zote mbili za *Fumo Liongo* na *Sundiata*.

5.2.3 Dhamira katika Tamthiliya Teule

Lengo mahususi la tatu lilikuwa linahusu kuchambua dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya za *Fumo Liongo* na *Sundiata*. Katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* kumejitokeza dhamira za uongozi kandamizi, rushwa katika jamii, usaliti, matabaka na nafasi ya mwanamke. Katika tamthiliya ya *Sundiata* kumejitokeza dhamira za uongozi mbaya, rushwa katika jamii, nafasi ya mwanamke na ushirikina katika jamii. Kwa jumla, matokeo haya ya utafiti yanaonesha kuwa kuna ufanano mkubwa wa dhamira katika tamthiliya teule kuliko zinavyotofautiana. Hata hivyo, dhamira ya uchawi na uganga inaonekana kujitokeza zaidi katika tamthiliya ya *Sundiata* kuliko katika *Fumo Liongo*.

5.3 Hitimisho

Kwa jumla tunaweza kusema kuwa, matumizi ya mbinu za Kiaristotle katika utunzi wa tamthiliya ni kitu ambacho hakikwepeki hata kwa tamthiliya za kimajaribio. Waandishi kama Ebrahim Hussein na Penina Mlama wamejitahidi sana katika kutunga tamthiliya ambazo zinafuata kanuni na misingi ya kijadi huku wakikwepa kanuni za Kiaristotle. Hata hivyo, hufika mahali wakajikuta tu bila ya kutaka wametumia kanuni za Kiaristotle katika utunzi wao. Mwandishi Emmanuel Mbogo kwa upande wake, yeye amejipambanua moja kwa moja kama mtunzi wa tamthiliya za Kiswahili anayezingatia kanuni za Kiaristotle katika utunzi wake wa tamthiliya. Pamoja na kutumia mbinu za Kiaristotle katika utunzi wake wa tamthiliya pia anatumia mbinu za kijadi za utunzi wa tamthiliya kama kuchanganya tanzu, wahusika wa kifasihi simulizi, majigambo na kadhalika. Hii ni sawa na kusema kuwa, utunzi wa tamthiliya kwa kuzingatia kanuni za Kiaristotle haumzui mtunzi kuingiza mbinu za kijadi katika utunzi wako.

5.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu tunapendekeza kuwa ni vema utafiti kama huu ufanywe katika kuchunguza tamthiliya nyingine za mwandishi huyu ambayo bado hazijatafitiwa. Hii itasaidia kuwa na uelewa mpana wa matumizi ya mbinu za Kiaristotle katika tamthiliya zote za mwandishi huyu.

Pia, tunapendekeza kuwa utafiti kama huu ufanywe katika kuchunguza matumizi ya mbinu za Kiaristotle katika tamthiliya za majaribio zikiwemo za Ebrahim Hussein na Penina Mlama. Hii itasiadia kufahamu makutano baina ya mbinu za Kiaristotle na zile za kijadi katika utunzi wa tamthiliya za Kiswahili.

MAREJELEO

Aristotle, M. (1958). *On Poetry and Style (Mh. G. M. A. Grube) the Bobbs Merrl Co. me* Indiana Polis New York.

Babbie, E. (1999), *The Basic of Social Research Balmont, Wads Worth,* Publishing Company.

Bertocini, E. 2 (1989). *Outline of Swahili Literature.* E.J. Brill Leidon.

Coombas, J. (1953). *Literature and Criticism Middlesex:* Chatto and Windus.

Creswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative and Methods Approches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Dorsch, S. T. (1965). *Aristotle/Harance/Longinus Classic Literacy Criticism Hardmads* Woths Penquin.

Raghwakul, T. (1990). *Department of English Meeru Collage Meeru,* Rama Brothers Education Publishers, Bank Street Koral Bagh, New Delhi 1005

Eliakim, K. K. (1987). *Misingi ya Maigizo,* Benedict Publication Ndanda Peramiho.

Etherto, M. (1982), *The Development of Africa Drama,* London Hutchinsan J. Company.

Grehani, H. (1957). *Afadhali Mchawi,* EALB Nairobi.

Grehani, H. (1957). *Mgeni Karibu,* EALB Nairobi.

Hussein, E. N. (1983). *Hatua mbalimbali za kubuni tamthiliya kufuatana na misingi ya Ki-Aristotle,* Makala ya Semina III Tuki Dar es Salaam.

Jonhson, C. (1978). *The Epic of Sundiata. An Attempt to define the model for Africa Epic Poetry PHD Dissertation,* Vols 1.4 Press.

John, J. W. (1956). *The Epic of Son – Jera,* Indiana University Press Bloomington.

Kihamba, A. (1980). *Hawala ya Fedha.* TPH, Dar es Salaam.

King'ei, G. K. (1987). *Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa Ebrahimu Hussein katika Mulika na 19.* Dar es Salaam TUKI

Kombo, D. K. and Tromp, D. L.A. (2006), *Proposal and Thesis Writing*: Kenya, Paulines Publucations Africa.

Kunene, M. (1979). *Emperor Shaka the Greate*: A zulu Epic London Heineman.

Ligembe, N. E. G. (1995). *The Uses of Metaphor in Penina Muhando's Lina ubani. A Stylistic Analysis.Tasnifu* ya Umahiri, (Haijachapishwa) University of Dar es Salaam.

Mbogo, E. (1993). *Matumizi ya Dhana na Sanaa katika Sanaa za Maonyesho Jadi katika tamthiliya ya leo katika Mulokozi na Mn'gong'o (wah)*: 181 206.

Mbogo, E. (1980a). *Giza Limeingia,* TPH Dar es Salaam.

Mbogo, E. (1980b). *Tone la Mwisho,* Dar es Salaam.

Mbogo, E. (1996). *Morani,* DUP Dar es Salaam

Mbogo, E. (1987). *Ngoma ya Ng'wanamalundi.* Education Service Center Dar es Salaam.

Mlama, P. M. (1983). *Utunzi wa Tamthiliya katika Mazingira ya Tanzania,* Makala za Semina III- TUKI Dar es Salaam.

Mofolo, T. (1981). *Chaka (Mf. D. Kunene)* Heineman London

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1979). *Mkwawa wa Uhehe* EAPH Nairobi.

Mutembei, A. K. (2012. *Korasi katika Fasihi Nadharia Mpya ya Uhakiki,* Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mwaifuge, E. S. (2001). “Beliefs and Human Behaviour in the Theatre of Ebrahim Hussein,” Unpublished M.A Thesis, University of Dar es Salaam.

Mwita, M. B. (2009). “*Uhakiki wa Mtindo na Maudhui katika Baadhi ya Tamthiliya za Penina Muhando (Mlama),*” Katika *Mulika* Na 28, Dar es Salaam: TATAKI. Kur 104-128.

Niane, D. T. 1979). *Sundiata,* An Epic of Old Mali Londong Longman.

Nicholous, A. (2011). “Ubuntu katika Tamthiliya za Penina Mhando,” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Owhinda B. O. A. (2002). *Ushairi wa Kiswahili na Ushairi wa Kilibya kufanana na kutofautiana. Tasnifu ya Uzamivu,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ramadhani, D. (2005). *The Uses of Metaphors in Mbogo’s Ngoma ya Ng’wanamalundi and Hussein’s Mashetani. A Stylistic Comparison.*Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa) University of Dar es Salaam.

Robson, C. (2007). *How to do a Research Project: A guide for Undergraduate Students*, Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Semzaba, E. (1997). *Tamthiliya ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Seydon (1982). *Cromment difener Ugenre epique un example La’popee* Africane Joinel Anthropoligical Society of Oxford XIII/A.

Shakesper, W. (1969a). *Tufani kilichotafsiriwa na S.S. Mushi,* Dar es Salaam Tanzania Publishing House.

Shakesper, W. (1969b). *Mabepari wa Venice (Tafsiri ya J. K. Nyerere)* Dar es Salaam Tanzania Publishing House.

Shakesper, W. (1969c), *Julius Kaizari (Tafsiri ya J. K. Nyerere)* Oxford University Press.

Sofokile, M. (1971). *Mfalme Edipode (Kilichotafsiriwa na S.S. Mushi)* Nairobi Oxford University Press.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya Historia na Maendeleo yake* Jomo Kenyatta Foundation – Nairobi.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Msingi na Vipengele vyake*, Phoenix Publishers Limited Nairobi Kenya.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi:* Nairobi, Vide Muwa.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Service and Research Enale Wood Chiffs.* Prentice Hall Inc.

Yin, R. K. (1994) *Case Study Research: Design and Methods*, (2^{nd} eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.